# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

## Episode 03: " Mjadala na Mdahalo"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA**

**List of characters for episode 3:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Harry, male (17)
- Layla, female (16)
- Roshi, female (16)
- Father Barnabus, Harry's uncle (49)
- Chief Dembele, Harry's father (51)
- Village men, women and children
- Students chatter on sports ground

1. **SIG TUNE**

2. **INTRO:**

**Hujambo na karibu kwa sehemu ya tatu ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga maisha yako katika makala hii ya "Daraja La Mto Gori"inayoeleza jinsi SIASA na DINI zinavyoweza kuigawanya jamii na kuzua uhasama baina ya Familia Mbili. Katika kipindi kilicho tangulia Vijana hawa walibaini kuwa kiongozi shuleni si sawa na kuwa kiongozi nyumbani. Katika makala ya leo"Mwanzo wa Mjadala" tutasikia jinsi Roshi anavyomhimiza Layla kuwa jasiri na kujiamini vilevile kuijua historia ngumu ya familia a Harry. Philip ni moja wa marafiki wakubwa wa Harry na anakusimulia hadithi hii.Tega sikio! .**

3. **SIG TUNE UP AND FADE**

4. **PHILIP/NARRATOR: Wazo la kuanzisha kikundi cha Majadiliano lilikuwa la mkurugenzi wa Chuo.Bibi Ayo Milulu alikuwa na azma ya chuo chake kiibuke washindi wa kinyang'anyiro cha kuwania kombe la mdahalo.Kwa sasa mabingwa watetezi ni shule ya sekondari ya Gori.Ingekuwa vyema kama wangeweza kuwapiku.Kwasababu ya hilo A.M kama tulivyomuita kwa jina lake la utani, aliwaita Layla na Harry viranja wa wanafunzi chuoni kuanzisha mikakati hiyo.Kwanza kabisa**

**wanahitaji ukumbi unaofaa wa kundi hilo jipya kukutana.**

**<u>Scene 1. In Ubuntu college</u>**

**Philip Narrator, Harry, Layla**

5. **<u>SFX: Sound of footsteps (2 people) walking down corridor, with a slight echo. Door opens</u>**

6. **HARRY:** **Hiki ni chumba cha Tatu, Unakionaje Layla? Kinaweza kufaa?**

7. **<u>SFX. Closes door. Inside room</u>**

8. **LAYLA:** **Mmm….. Ni kizuri nimekipenda…! Ni kizuri kuliko vyumba vyengine tulivyoviona.Nayapenda madirisha yake!**

9. **HARRY:** **Ndio, madirisha yake yatatupa mwongozo na mwanga zaidi wakati wa mijadala yetu! *(laughs)* Na A.M. anataka orodha ya mada tutakazozijadili muhula huu.**

10. **LAYLA:** **Itakuwa bora tukiwashirikisha wanafunzi wengine.*(Excited.)*Harry Waonaje tukiwapa orodha ya masuali?**

11. **HARRY:** **Orodha ya aina gani?**

**12. LAYLA:** **Kama ile inayowataka wanafunzi kukiandika wanachokipa umuhimu maishani mwao.**

**13. HARRY:** **Hilo ni Wazo zuri sana Layla…, Na naliunga mkono .. nadhani sote tutaifurahia shughuli hiyo.**

**14. PHILIP/NARRATOR: Harry alikuwa na furaha ilioje kupata fursa ya kufanya kazi na Layla .Uso mzima ulijawa bashasha.Hilo lilinichukiza sana…! Kila wakati nilikuwa nikiwaza kuwa nilistahili kuipata nafasi hiyo.Niliamini kuwa Babangu alifanya kila njia kuwashawishi niteuliwe! Ukweli wa mambo ni kuwa mkurugenzi A.M tayari alimchagua Harry na sina budi kuukubali uamuzi huo.Sasa ikiwa nataka kuwa na ukaribu na Layla, njia pekee ni kujiunga na Kundi la mjadala. Na nilijisajili! Pia kwenye klabu ya spoti ambako nilipata nafasi ya kumtazama Layla kwa karibu akifanya mazoezi na rafiki yake Roshi kama alivyomtazama mdogo wake Hassan akiwa pembeni.**

<u>**Scene 2. On the sports track**</u>

**Roshi, Layla, Philip Narrator**

**15. <u>SFX: Sport track, birds, students running in the background, students chatting and talking from a distance</u>**

**16. ROSHI: *(panting)* Layla, Naona Hassan anatutazama sana. Yule kijana anasumbuliwa na nini lakini?**

**17. LAYLA:** ***(panting)*** **Ananisubiri tuandamane kurudi nyumbani , Roshi. Hapendi kabisa kuniona hapa- Fikra zake zinamtuma kuwa wasicha wa kiislamu hawapaswi kushiriki michezoni**.

**18. ROSHI:** **Huo ni Upuuzi-wasichana wengi tu wa Kislamu wanashiriki michezoni Ulimwenguni. (panting)… Ehh kwa hivyo Layla tumechukua muda gani kukimbia mzunguko huu?**

**19. <u>SFX: Stopwatch</u>**

**20. LAYLA:** **Dakika 3 sekunde 21 nukta 8**.

**21. ROSHI:** **Muda mzuri sana! Tafadhali mwambie yule Kakako aachane na sisi kabisa, Si vizuri anavyofanya.!**

**22. LAYLA:** **Nimejaribu kumweleza lakini ni kama hataki kunielewa. Unajua Mamangu alikuwa akiniambia hadithi kuhusu Mtume Mohammed alivyokuwa akifanya mazoezi na kushiriki michezo ya aina mbali mbali. Alipenda sana mchezo wa Masumbwi, kurusha mishale na hata mashindano ya Farasi. Alikuwa akishindana na mkewe Aisha**

na wakati mwingi Aisha alikuwa akishinda.!.Hassan anapaswa kufahamu kwamba michezo haiendi kinyume na mafundisho ya Kiislamu. Lakini Roshi, unajua hajakosea kote. Ni kweli dini ya Kiislamu ina sheria kali, mfano mavazi unayovaa, sehemu ya kubadilishia mavazi hayo na rafiki unayeandamana naye uani.

23. ROSHI: Hebu tazama,- mikono na miguu yako imefunikwa… kama mimi tu!

24. LAYLA: Ni kwweli .. nasumbuka na joto..!, Tunakufa kwa joto.

25. ROSHI Tunapasa kumuuliza mwalimu wetu wa mazoezi aturuhusu kuvalia mavazi ya michezo mepesi kidogo hususan kwa Wasichana wa kiislamu. Hijab,.. kitambara cha kufunika kichwa na shingo. hiyo inakubalika…! Na pia mahali pa kubadilisha mavazi yetu, tunaweza kuruhusiwa kwenda nyumbani kubadilisha nguo zetu huko na kurejea.

26. LAYLA: Lakini tutakosa umbea,gumzo na vicheko vya wasichana kawaida wanapokwenda

| | |
|---|---|
| | **kuoga uani..! Aiii… hapana …! Wewe pia ni Musilamu.Mbona mtazamo wako uko tofauti kuhusu suala hili?Kwanini huingii wasiwasi mwili kuonekana na wasio waislamu?** |
| **27. ROSHI:** | **Tuna mitazamo tofauti kwetu. Mamangu anaamini kwamba Kuwa mwanamke na jasiri anayeupa changamoto mfumo dume ndio jambo muhimu katika ulimwengu wa sasa..!. Kwanza lazima tufahamu kwamba sisi ni Wanawake, kisha pili ..Waislamu!** |
| **28. LAYLA:** | **Lakini hilo halinisaidii mimi hata kidogo! Sasa Niambie nitafanya nini kuhusu tabia ya Hassan na marafiki zake wa Madrassa…? Kama unavyojua chuo cha Madrassa kina sheria kali..** |
| **29. ROSHI:** | **Kuwa na ujasiri msichana ,..na ujaribu kuwapa changamoto! Sio hao waliopewa wajibu wa kudumisha mienendo ya Waislamu wengine. Kakako ana umri wa miaka 12 pekee na mwambie hata Palestina na Jordan wana timu za kandanda za wanawake. Na hawajavunja sheria yoyote ya Kiislamu..!,na hata wewe pia.** |
| **30. LAYLA:** | Ingekuwa bora **pia nikimuonyesha picha ya Nawal El Moutawake, mwanamke wa** |

**kwanza Muislamu kushinda nisha ya dhahabu kwenye michezo ya Olimpiki ya Los Angeles mwaka wa 1984. Ulikuwa ushindi mkubwa sana kwa wanawake , na mimi pia nataka kuiga mfano wake kushinda mbio za mita 400 kuruka vihunzi katika mishindano yajayo ya Olimpiki!**

**31. ROSHI:** **Jipe moyo Layla,! Sasa njoo hapa tushindane kukimbia hadi uani!**

**32. <u>SFX: Layla and Roshi sprinting away, laughing and joking</u>**

**33. PHILIP/NARRATOR:** **Nilisimama na kuwatazama wasichana hao wawili warembo wakikimbia. Wakati huo huo wikiendi ilikuwa inanukia,na tayari Harry alikuwa ameanza kujiandaa kumtembelea Babake kijijini akiandamana na babake mdogo Kasisi Barnabus. Kwa kuwa ni Mtu anayeheshimika, wanakijiji walimsubiri kumkaribisha kwa hamu kasisi Barnabus, na hata Harry ambaye alikuwa amechaguliwa kuwa kinara shuleni mwao.**

**<u>Scene 3. Outside in the village</u>**

**Adult voices, Chief Dembele**

***34. <u>SFX: Village sounds. Cows/birds. Women singing and ululating</u>***

**35. M/F ADULT VOICES: Karibu nyumbani….! Karibu sana Kasisi Barnabus..! Karibu Harry karibu nyumbani…!**

**36. CHIEF Dembele: Barnabus, Harry! Karibuni ndani…. Angalau mpate vinywaji .**

**<u>Scene 4. Inside hut</u>**

**Chief Dembele, Father Barnabus, Harry**

**37. <u>SFX: Footsteps, rustle of clothes / sitting - Glasses, pouring water.</u>**
**<u>In the background: village sounds.</u>**

**38. CHIEF: Tafadhali kaeni chini mupate kinywaji. Nimefurahi sana mumetutembelea tena.**

**39. FATHER B.: *(drinking water)* Ahsante Kaka….**

**40. HARRY: *(drinking water)* Ahsante Baba….**

41. ***(OPTIONAL) FADE BACKGROUND CONVERSATION: Improvise polite exchange of talk about weather, village, cows, life in the town, Father Barnabus's work in the town, his business interests...***

42. ***FADE UP VILLAGE SINGING - CROSS FADE WITH CONVERSATION BELOW***

43. **CHIEF:** Enhe nieleze hii nafasi ya Kiranja hasa ina umuhimu gani? **mwanangu?**

44. **HARRY:** **Mradi wetu mkubwa wa kwanza Baba, ni kuanzisha kundi la mjadala na mdahalo.** ***(After a pause - hesitating)*** **Na nitashirikiana kwa karibu na Layla Omer..**

45. **CHIEF:** ***(Clearing his throat)*** **Familia ya Omer imekuwa mahasimu wa familia hii ya Dembele.Familia zetu zimekuwa na historia ya uhasama mkubwa.**

46. **HARRY**: **Sikulifahamu hilo kabisa… chanzo chake ni nini Baba?**

47. **CHIEF**: Ardhi.Suala la ardhi husababisha uhasama wakati wote.Hata sasa bado ni hivyo**!**

**48. FATHER B.:** **Baraza la waislamu linataka kujenga msikiti katika kipande cha ardhi ambacho sisi wafuasi wa kanisa Katoliki tunakitaka kwa ujenzi wa kanisa. Mimi na Ishmail Omer ni wanachama wa kamati kuu ya maendeleo ya mji huu na aghlabu tuna mitazamo tofauti kuhusu aliye na haki ya kujenga kwenye kiwanja hicho.**

**49. HARRY**: ***(agitated)*** **Lakini mzozo huo unatuhusu vipi mimi na Layla? Hatuhusiki kamwe….. na …na mzozo huo. Mimi ni kiranja wa kiume na yeye wa kike, na tumeagizwa kupanga mikakati ya kuanzisha klabu hii shuleni. Mkurugenzi anataka tushirikiane ili kuufanikisha mradi huu, …sasa wataka mimi nifanyeje baba?**

**50. CHIEF:** **Harry, mwanangu …. Unaweza kushirikiana na LAYLA Omer lakini katika mazingira ya shuleni pekee ..!** ***(Pause)*** **Na kwanza hebu niambie ..msichana huyu..ni Mrembo…?**

**51. HARRY:** **Saana !**

**52. CHIEF:** **Kumbe…!.**

**53. FATHER B:** **Unajua mimi nilitaka sana ulifikire wazo la ukasisi Harry!.**

**54. HARRY**: **Baba Mdogo, sio hivyo, mimi bado ni mdogo, nina miaka kumi na saba tu.Bado sijaamua nitafanya nini maishani.Bado nasoma katika shule hii isiyojikita katika madhehebu ya aina yoyote. Na hivyo ndivyo ulivyotaka Baba, Sivyo?.Hata wewe uliamua kutokuwa kasisi na badala yake ukaamua kuoa wake wawili**.

**55. CHIEF**: **Ni kweli mwanangu , hilo ni sehemu ya wajibu wangu kama Chifu.Wanakijiji wananitarajia nioe wake wawili au hata watatu. Babangu na hata Babu yangu walioa zaidi ya mke mmoja,kwani ni ishara ya ufanisi na mamlaka.**

**56. FATHER B**: **Nilijaribu kumshawishi Babako ajiunge na ukasisi miaka mingi iliyopita bila mafanikio!U*seja* ni sehemu ya wajibu wangu kama kasisi wa kanisa katoliki. Hii inakupa fursa ya kuyazingatia mafundisho ya dini. Kila mtu huwa tofauti Harry!**

**57. CHIEF:** **Tunaheshimiana licha ya maamuzi tofauti maishani.Harry lazima uamue hatima ya maisha yako ila tunawajibu wa kukuongoza.**

**58. FATHER B.:** **Na katika njia ambayo haitauchochea mvutano katika ukoo wetu.**

**59. HARRY:** **Kwahiyo unapendekezo gani?**

**60. FATHER B:** **Hakuna kushirikiana naye nje ya mazingira ya shule. Na pia tunayoyazungumzia hayamhusu.. sawa?**

**61. CHIEF:** **Kakangu, lengo kubwa maishani ni kuleta uelewano na sio kuchochea mizozo.Nafikiri Harry na Layla wanapasa kuonyesha mfano mzuri wa uongozi shuleni, na kuudhihirishia uongozi wa shule kuwa haukufanya makosa kuwachagua hao wawili ..**

**62. HARRY:** **Basi pia lazima tutafute njia ya kuusuluhisha mzozo uliopo baina ya familia hizi.**

**63. CHIEF:** **Viongozi wazuri husameheana. Viongozi bandia huchochea uhasama usio na maana yoyote, uhasama wa kikabila, ukoo, rangi na hata dini. Na hilo linaweza kutendeka**

**hapa hapa Gori! Mzozo baina ya Waislamu na Wakristo,kwa kisingizio cha kung'ang'ania kipande cha ardhi tu!...**

**64. SIG. TUNE UP**

**65. OUTRO:**

**Na hadi hapo msikilizaji tumefika mwisho wa kipindi cha leo cha Noa Bongo Jenga Maisha yako..Layla sasa amejitolea kuendelea kufanya mazoezi ya kukimbia naye Harry anakabiliwa na changamoto mpya .Ungana nasi kwa sehemu ya nne katika mchezo huu wa Radio "Daraja la Mto Gori" ufahamu mengi zaidi wakati Harry na Layla wanapokumbana na misukosuko ya urafiki. Na kumbuka ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.**

**END OF EPISODE 3**